TANGAZO LA SERIKALI NA. 217 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 275 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Songwe ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Songwe ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 6

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 6 kwa-

(a) kufuta kanuni ndogo ya (1) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(1) Halmashauri itahakikisha kwamba ada au ushuru unakusanywa wakati wote katika maeneo yake.";

(b) kufuta kanuni ndogo ya (2); na

(c) kubadili mpangilio wa kanuni ndogo za (3) na (4) kuwa kanuni ndogo za (2) na (3) mtawalia.

Marekebisho ya kanuni ya 10

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 10 kwa kufuta kanuni ndogo ya (5) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(5) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo za (3) na (4), kabla ya Halmashauri kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa

ya maandishi ya muda usiopungua siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka, na siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, kwa mdaiwa na umma kuhusu kusudio la kuuza mali hizo.”.

Marekebisho katika Jedwali la Kwanza

4. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza-

(a) katika Sehemu ya Kwanza, kwa kuongeza maneno “kwa Mwaka” mara baada ya neno “(Shilingi)” lililopo katika safu ya tatu ya mstari wa kwanza; na

(b) katika Sehemu ya Saba A, kwa kuondoa neno “viwanja” lililopo katika safu ya pili ya kipengele cha 16 na badala yake kuweka maneno “viwanda vikubwa”.

Dodoma,
10 Januri, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*